


CHANGAMOTO >> Umepungua kutoka tani 120 hadi 20

# Uzalishaji minofu ya sangara wapungua

**Na PETER KATULANDA**, *Mwanza*

UZALISHAJI katika viwanda vya kusindika minofu ya samaki aina ya sangara, jijini Mwanza, umeshuka kwa miezi minane sasa, kutoka wastani wa tani 120, kwa siku hadi kufikia tani 20, kutokana na uhaba wa samaki hao.

Uhaba huo umefanya wavuvi wauze samaki hao katika soko jingine la ndani, kwa kutengenisha bondo na samaki na kupata faida zaidi, badala ya kuuzia viwanda hivyo, ambavyo hununua sangara mzima (akiwa na bondo) kwa bei ndogo.

Kutokana na hali hiyo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka wamiliki wa viwanda vya kusindika minofu ya samaki jijini hapa, kuzitafutia ufumbuzi sababu zinazochangia wavuvi kuuza samaki hao katika soko la ndani, badala ya viwandani kwao.

Ulega, alitoa agizo hilo juzi, alipotembelea viwanda vya samaki vya Victoria Perch na Tanzania Fish Processors, na kuelezwa changamoto ya upatikanaji wa malighafi ya samaki hao, ilivyochangia kushuka kwa uzalishaji.

"Ni lazima make, mjadili mnafanyaje kutanzua hiki kitendawili. Wavuvi wanaona bora wauze samaki wao kwenye soko la ndani, badala ya kuuzia viwanda vyenu," alisema.

Naibu Waziri, alieleza kuwa soko la ndani linamfanya mvuvi atenganishe bondo la samaki na samaki mwenyewe na kuviuza tofauti, hali inayompatia faida zaidi kuliko kuuza viwandani samaki mzima pamoja na bondo kwa bei ileile.


Awali, Meneja Ubora wa Victoria Perch, Edwin Okong'o, alisema kwa miezi minane sasa, uzalishaji wa minofu ya samaki umepungua kutoka asilimia 120, kwa siku, hadi kufikia asilimia 20, kutokana na uhaba wa sangara uliotokana na mabadiliko ya hali hewa na mvua kubwa.

Meneja Rasilimali Watu wa Tanzania Fish Processors, Godfrey Samwel, alisema upungufu wa sangara, umeathiri shughuli za kiwanda chake huku uvuvi haramu ukichangia upungufu huo.

"Tunaiomba serikali iendelee kukabiliana na uvuvi haramu, hasa kwenye mialo, maana pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa, unachangia upungufu wa samaki," alisema Samwel.

Ofisa Uvuvi wa Jiji la Mwanza, Kennnedy Kitinusa, alisema uhaba wa samaki viwandani, umetokana na sababu mbalimbali, ikiwemo uvuvi wa kutumia zana haramu, kutoweka kwa samaki aina ya sangara, kulikotokea Februari, mwaka huu, pamoja na bei inayotolewa na viwanda hivyo.

USHIRIKA



NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akikagua boti za Chama cha Ushirika wa Wavuvi Zilagula, akiwa ziarani kwenye Kisiwa cha Zilagula, Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza. Chama hicho kimepata mkopo wa sh.milioni 100.7, kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). (Na Mpigapicha Wetu).

## TRA yawaondoa hofu wafanyabiashara

**NA ANGELA SEBASTIAN**, *Bukoba*

WAFANYABIASHARA Mkoa wa Kagera wametakiwa kubadili mtazamo hasi wa kudhani washauri wa mahesabu wanaotambuliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), mkoani humo, wanashirikiana na maofisa wa mamlaka hiyo kuwakandamiza.

Ushauri huo ulitolewa Meneja Ukaguzi wa TRA, Calist Lyimo, wakati wa kikao kati ya mamlaka hiyo na wafanyabiashara, kilicholenga kusikiliza na kutatua kero zao, kilichofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita, mjini Bukoba.

Akizungumza katika kikao hicho, Katibu wa Chama cha Wafanyabiashara Wakulima na Wenye Viwanda (TCCIA), mkoani Kagera, Ladislaus Rwechungura, alisema yapo mambo kadhaa yanayofanywa na baadhi ya washauri hao, ikiwemo kuwanyanyasa wafanyabiashara na kutowatendea haki.

> **"Yapo mambo kadhaa yanayofanywa na hawa washauri mnaowatambua TRA, lakini hamuyaoni. Kumbukeni mshauri ni mtaalamu, hawezi kuwatendea haki wafanyabiashara. Hizi ndizo shida za nchi zetu za dunia ya tatu.**
>
> Katibu Chama cha Wafanyabiashara Wakulima na Wenye Viwanda (TCCIA), Ladislaus Rwechungura

"Yapo mambo kadhaa yanayofanywa na hawa washauri mnaowatambua TRA, lakini hamuyaoni. Kumbukeni mshauri ni mtaalamu, hawezi kuwatendea haki wafanyabiashara. Hizi ndizo shida za nchi zetu za dunia ya tatu," alisema.

Aliongeza: "Tumuache huyu mfanyabiashara alipe kodi halali ya serikali inayojulikana, na yeye abaki na faida ili kumsaidia asimame na kuendelea na biashara."

Scanned with CamScanner

Nipashe Uk.8 Mei 27,2021

# Ulega autaka ushirika matumizi vyema boti za mikopo ya TADB

**Na Mwandishi Wetu,** SENGEREMA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi Abdallah Ulega, amekitaka Chama cha Ushirika cha Zilagula wilayani hapa kutumia vyema mkopo uliotolewa na

Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kujenga boti za kisasa, ili zisaidie viwanda vya samaki jijini Mwanza kupata malighafi kwa wakati na kwa uhakika.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, baada ya

kuridhishwa na ujenzi wa boti tatu za kisasa za uvuvi, kati ya boti

tano ambazo zinajengwa kwa mkopo wa Sh. milioni 100.7 ambao umetolewa

TADB kwa chama hicho, Ulega alisema fedha hiyo ni mkakati wa serikali wa kuwapatia wavuvi vyombo vya kisasa na kwamba matumizi mazuri ya boti hizo utavifanya viwanda kupata malighafi kwa uhakika na

pia kuifanya sekta ya uvuvi kutoa mchango mkubwa zaidi kwenye pato la taifa.

"Mpango wa serikali ni kuona sekta ya uvuvi inatoa mchango zaidi katika ukuaji wa pato la taifa na ndiyo ili muweze kupata boti za kisasa zitakazowasaidia kufanya vyema shughuli zenu," aliwaeleza wanaushirika hao na kuongeza ni vyema mkopo huo ukatumika vizuri na marejesho yake yafanyike kwa

wakati.

"Kilio cha wavuvi wengi ni walanguzi wanaowanyonya. Walanguzi wamekuwa wanufaikaji wakubwa wa nguvu ya mvuvi. Uwapo wa boti hizi utawezesha kupata samaki wengi zaidi ambao watauzwa kwa bei nzuri kwa sababu samaki wanahitajika katika soko la ndani na nje ya nchi," alieleza.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema benki yao itaendelea kufanyia kazi chang moto zote zinazojitokeza ikiwam kukosekana kwa mikopo kwa ba dhi ya vyama vya ushirika licha y kufuata taratibu zinazotakiwa.

"Mwanzoni tuliwaomba wav waunde vyama vya ushirika ili u weze

kuwapa mikopo. Tunashuku kwa sababu mwitikio umeku mkubwa na hivyo kurahisisha k ya kuratibu mikopo inayotolewa benki," alisema.

Scanned with CamScanner

The Guardian May 27,2021 NATIONAL.NEWS




Livestock and Fisheries deputy minister Abdallah Ulega pictured yesterday inspecting boats for Sengerema District's Zilagula cooperative society built with a 100.7m/- loan from ythe Tanzania Agricultural Development Bank. Photo: Guardian Correspondent

Scanned with CamScanner

The Guardian Uk.7, May 27,2021



Karatu District Commissioner Abbas Kayanda inspects goats rearing project at Chemchem village in Arusha Region. Photo: Correspondent Woinde Shizza

Scanned with CamScanner




NMB Bank Plc acting chief of internal audit department Benedicto Baragomwa (R) shakes hands with a representative of Arusha District Commissioner Allan Rushokana (3rd L) after the launch of motorbikes loans project in the northern zone yesterday. Others are from left head of NBM Bank business banking Alex Mgeni, Motornike riders association chairman Okero Costantine (2nd L) and motorbike rider Stella Nguma (R). Photo: Guardian Correspondent

# Ulega implores Zilagula cooperative to ensure steady flow of fish to industries

**By Guardian Correspondent, Sengerema**

Livestock and Fisheries deputy minister Abdallah Ulega has implored Zilagula cooperative society in Sengerema District to use gainfully modern fishing boats they have acquired by loans and ensure Mwanza fish industries get improved flow of fish to enable them maintain their production operations.

Talking to members of the cooperative here after inspecting three, out of the five boats, being built with the help of the 100.7m/- loan from the Tanzania Agricultural Development Bank (TADB), Ulega said he was satisfied with the quality and performance of the boats and urged the cooperative to make most of the loan, improve the livelihoods of members and ensure steady flow of fish to the industries.

He said steady flow of the raw material to the industries will guarantee the cooperative a secure market, save members from adverse ploys of middlemen and will also translate into increased contribution of the fisheries sector to the national economy.

He urged Mwanza Region fishermen to form cooperatives to become creditworthy and access loans from financial institutions.

"The loud cry we have heard is that fishermen are losing to middlemen in broad daylight. Form cooperatives to eliminate middlemen; to be able to get loans from financial institutions and have guaranteed markets. This is my appeal to all Mwanza Region fishermen," he pleaded.

TADB managing director Japhet Justine said the bank is aware of the fact that cooperatives have always been unable to get loans from financial institutions even after meeting all requisite conditions.


He assured the audience that their bank will continue solving challenges the cooperatives are facing. In the past, he said, the bank had difficulty in persuading prospective borrowers to form cooperatives but now the trend is changing for the better.

The chairman of the cooperative, Joram Yuda, thanked the government for remaining steadfast in making pro-poor reforms and cleansing the cooperative movement. "These boats are a glaring evidence of the government's efforts to ensure cooperatives in strategic sectors like agriculture, livestock and fisheries are creditworthy and win the confidence lenders," he said.

Scanned with CamScanner

**Maelekezo>> Kipaumbele kitolewe shughuli za utafiti na ugani**

# CCM yainyooshea kidole bajeti Wizara ya Mifugo



Na JUMA ISSIHAKA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeielekeza serikali kuboresha maeneo saba ya kipaumbele katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kupitia bajeti ya mwaka 2021/22, kwa lengo la kuleta mabadiliko makubwa na ya kisayansi katika ufugaji, yatakayomgusa mfugaji.

Aidha, imeipongeza serikali kwa utekelezaji wa maelekezo ya Katibu Mkuu, Daniel Chongolo, aliyoyatoa kwa Wizara ya Kilimo, Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Nishati, ambapo alizitaka kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025.

Akibainisha maeneo hayo, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema serikali inapaswa kuzipa kupaumbele shughuli za utafiti na ugani, kwa kuviwezesha vituo kufanya kazi zao kwa kufuata ajenda ya kitaifa.

Alisema uanzishwaji huo ni wa madarasa ya mifugo katika halmashauri mbalimbali nchini, ili wafugaji wajifunze ufugaji wa kisasa na wa kibiashara, pia kuwepo kwa maofisa ugani kila ngazi, wawezeshwe usafiri wa magari na pikipiki.

Eneo jingine, alisema ni uanzishwaji wa mifugo na masoko ili kuwa na maziwa na nyama bora, kukidhi soko la ndani na nje, hivyo serikali inapaswa kuimarisha vituo vya uhimilishaji kufikia walau 1,000,000 na kuwajengea uwezo wahimilishaji katika halmashauri zote.

Pia, CCM ameielekeza serikali kununua mitamba 500, kwa ajili ya mashamba ya kuzalisha mifugo ya serikali kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa mitamba.

Mbali na hilo, alisema serikali kupitia Taasisi ya Mifugo (TALIRI), iendeleze tafiti za uzalishaji wa kuku wa kienyeji, kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa vifaranga wa kienyeji bora nchini.

> Mbali na hilo, alisema serikali kupitia Taasisi ya Mifugo (TALIRI), iendeleze tafiti za uzalishaji wa kuku wa kienyeji, kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa vifaranga wa kienyeji bora nchini

Shaka, alitaja eneo la tatu kuwa ni serikali kutilia mkazo biashara ya mifugo na mazao yake, kwa kujenga na kukarabati minada ya mifugo.

Pia, kufanya mapitio ya ada na tozo mbalimbali, hususan tozo ya thamani ya mizigo na kuondoa zisizo za lazima, kwa nyama zinazouzwa nje ya nchi baada ya ukaguzi wa mifugo.

Kuhusu eneo la malisho na maji, Shaka alisema CCM imeilekeza serikali kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa, kutenga maeneo ya malisho, kuimarisha na kujenga miundombinu ya maji.

Akizungumzia migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, alisema serikali itafute ufumbuzi wa kudumu wa migogoro kwa kuzingatia maslahi ya pande zote.

Katika sekta ya uvuvi, Shaka alisema inayo nafasi kubwa ya kuchangia pato la taifa na kukuza ajira, ustawi wa watu na utoshelevu wa mahitaji ya samaki nchini, hivyo serikali iandae mipango ya ujenzi wa bandari ya uvuvi katika ukanda wa Pwani, kuwezesha meli za uvuvi kutia nanga.

Kadhalika, alisema CCM inaielekeza serikali kukarabati na kupanua vituo vya kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki.

Eneo la mwisho, alisema serikali inapaswa kutilia mkazo suala la elimu na mafunzo kwa wavuvi, kusaidia uvuvi endelevu na kusaidia vizazi vya sasa na vijavyo, kadhalika kupunguza malalamiko ya wavuvi.

Vilevile, alisema CCM imeishauri bajeti ya wizara hiyo, sekta ya uvuvi iangaliwe upya kwa kuwa hakuna vipaumbele vinavyomgusa mvuvi moja kwa moja.

## Dk. Mwinyi ajivunia Serikali ya Umoja wa Kitaifa Z'bar

Na MWANDISHI WETU

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema hatua ya kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), imelenga kuwawezesha wananchi kuishi kwa amani na utulivu, hivyo kuharakisha kasi ya maendeleo.

Dk. Mwinyi, alisema hayo jana, Ikulu, jijini Zanzibar, alipozungumza na Uongozi wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, uliomtembelea ofisini kwake.

Alisema uundwaji wa SUK, umeibua ufumbuzi wa changamoto za kisiasa zilizoikabili Zanzibar, na kusisitiza kuwa serikali yake itaweka nguvu katika kuyapatia ufumbuzi matatizo ya wananchi, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi alizozitoa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Aliahidi kushirikiana na tume hiyo kufanikisha vyema majukumu yake na kutimiza matakwa ya kikatiba.

Rais Mwinyi, alipongeza tume hiyo kwa kuweka mfumo mzuri wa mawasiliano ya kimtandao na kuwafikia wananchi wengi.

Alisema serikali imeshalipatia ufumbuzi suala la kuwepo uwiano wa nafasi za ajira kati ya vijana wa Tanzania Bara na Zanzibar, kupitia vikao vya Kamati ya Muungano, ambapo sasa Zanzibar itapata wastani wa asilimia 21 ya nafasi katika sekta za Muungano.

Scanned with CamScanner